# Mchango wa Tanzu za Kimaigizo za Fasihi Simulizi katika Umahuluti wa Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi wa Riwaya ya *Mafuta*

*Simiyu Benson Sululu[1], Richard Makhanu Wafula[2] na Joseph Nyehita Maitaria[3]*
[1]*Chuo Kikuu cha Kibabii*
[2]*Chuo Kikuu cha Kenyatta*
[3]*Chuo Kikuu cha Karatina*

**Ikisiri**

**Riwaya ni mojawapo ya tanzu za fasihi andishi ambazo zimepiga hatua kimaendeleo katika uandishi wake. Mathalan, riwaya ya Kiswahili imeandikwa na waandishi ambao ni Waswahili na ambao si Waswahili. Kwa hivyo, riwaya ya Kiswahili inaeleza tajriba ya Waswahili na Waafrika wengine wasiokuwa Waswahili. Mazingira wanamotoka waaandishi wa riwaya ya Kiswahili, wasiokuwa Waswahili, yamechangia na kuathiri uandishi wao. Waandishi hawa wameingiza vipengele vya fasihi simulizi na utamaduni wa jamii zao katika riwaya za Kiswahili wanazoandika. Makala haya yanalenga kuchunguza jinsi uingizaji wa vipengele hivi vya fasihi simulizi za watunzi wa riwaya ya Kiswahili, wasiokuwa Waswahili, unachangia umahuluti wa riwaya hii. Mahsusi, makala haya yamedadavua mchango wa tanzu za kimaigizo za fasihi simulizi katika umahuluti wa riwaya ya Kiswahili kupitia mfano ya riwaya ya *Mafuta* iliyoandikwa na Katama Mkangi. Uchunguzi huu umefanywa kwa kutumia Nadharia ya Umahuluti wa Utamaduni inayoshikilia kwamba panapotokea hali ya mtagusano baina ya tamaduni tofauti, matokeo yake si wingi-tamaduni bali ni mchanganyiko wa vipengele kutoka tamaduni hizi ambao zao lake huwa na sifa za kimahuluti. Nadharia hii imetumiwa kufafanua jinsi umahuluti wa riwaya ya Kiswahili umechangiwa na uingizaji wa vipengele vya tanzu za kimaigizo za fasihi simulizi kutoka jamii ya mtunzi teule ambaye si Mswahili. Katika kufanya hivyo, makala haya yamebainisha jinsi riwaya ya Kiswahili ilivyo nyumbufu kwa ambavyo inajumuisha vipengele kutoka asili anuai ambavyo vinaifanya kuwa changamano na ya kimahuluti.**

**Maneno Muhimu:** *Waswahili, Riwaya ya Kiswahili, Tanzu za Kimaigizo, Unyumbufu, Umahuluti*

**Utangulizi**

Ipo idadi kubwa ya waandishi kutoka jamii zisizo Waswahili, ambao wameandika riwaya ya Kiswahili. Dhana 'Waswahili' katika muktadha wa makala haya inarejelea wazawa wa lahaja mojawapo za Waswahili na ambao wanatumia mojawapo ya lahaja za Kiswahili kama lugha yao asilia. Inafuatia basi kwamba, wapo watunzi wa riwaya ya Kiswahili ambao ni Waswahili na wengine, kama vile Katama Mkangi, ambao si Waswahili. Nayo riwaya ya Kiswahili katika muktadha huu ni riwaya ambayo utunzi wake unatilia maanani mikatale na mfumo wa lugha ya Kiswahili. Waandishi wa riwaya ya Kiswahili wasiokuwa Waswahili, wameendelea kutumia maudhui, ploti na vipengele vingine vya tamaduni na fasihi simulizi za jamii zao katika kuendeleza kazi bunifu za Kiswahili. Kulingana na Sululu, Wafula na Maitaria (2021), hali hii imechangiwa na sababu kwamba waandishi hawa wanatoka katika jamii ambazo zina tamaduni na fasihi simulizi maalum. Kwa misingi hiyo, watunzi wa riwaya ya Kiswahili kutoka mojawapo ya jamii hizi wanapofanikisha usanii wao, huenda wakaathiriwa na fasihi simulizi za asili zao. Kama anavyoeleza Mlaga (2017), athari ni hali ambayo hutokea katika viwango anuwai baina ya wanadamu mathalan baina ya mataifa, baina ya vipindi tofauti vya wakati, baina ya tanzu tofauti za kisanaa na hata baina ya fasihi na taaluma zingine. Athari hizi zinapelekea hali ambapo riwaya ya Kiswahili iliyoandikwa na watunzi hawa haiwi halisi tena. Ni riwaya ambayo imejumuisha vipengele anuwai vikiwemo tanzu za fasihi simulizi kutoka jamii za watunzi wake. Mojawapo ya tanzu hizo ni utanzu wa kimaigizo. Maigizo husheheni vitendo na msururu wa matukio yanayoibua hisia za washiriki (Maritim, 2012). Maigizo haya hutokea katika

muktadha wa matukio ya kitamaduni yanayohusisha shughuli mbalimbali za maisha ya kila siku ya wanajamii.

Makala haya yameangazia tanzu za kimaigizo za fasihi simulizi katika muktadha wa miviga ya kitamaduni kama inavyotekelezwa katika jamii ya Waribe, anakotoka Katama Mkangi. Aidha, makala haya yametathmini jinsi mwandishi huyu alivyoingiza baadhi ya vipengele vya maigizo ya fasihi simulizi ya jamii yake katika riwaya yake teule ya Kiswahili na hivyo kuchangia umahuluti wa riwaya hiyo na riwaya ya Kiswahili kwa ujumla.

**Dhana ya Umahuluti**

Umahuluti unahusu mchanganyiko wa vipengele kutoka tamaduni mbalimbali. Matokeo yake, kulingana na Sululu (2021), ni utamaduni usio na udhu; utamaduni unaojumuisha mseto wa vipengele vinavyotokana na tamaduni mbalimbali vinavyoufanya kuwa thabiti zaidi. Umahuluti basi ni zao la hali ambapo watu kutoka asili mbalimbali huingiliana na kuathiriana ili kujenga miundo mipya ambayo ni bora zaidi. Kwa mujibu wa Bhabha (1994), hii ina maana kwamba umahuluti hauleti mambo hasi kama vile udhalili, uchafuzi, uchotara na upotovu kama ilivyosawiriwa katika nadharia za kijamii katika karne ya tisa bali una mwelekeo chanya kwa sababu zao linalotokea linaweza kuwa na nguvu fulani inayolifanya kuwa hata bora zaidi.

Katika fasihi, umahuluti hudhihirika kupitia kazi za waandishi wanaotoka katika tamaduni tofauti. Kama anavyoeleza Okwena (2019), hali hii hutokana na mchanganyiko wa jamii-lugha mbili ndani ya mipaka ya usemi mmoja. Matokeo yake ni mchanganyiko wa mawazo na mitindo kutoka asili tofauti katika kazi ile ile ya kisanaa. Naye Obiechina (1975), akiandika kuhusu riwaya ya Kiingereza ya watunzi kutoka Afrika Magharibi, anaeleza kuwa upekee huo umechangiwa na mchanganyiko wa tamaduni, jadi na mazingira ya eneo wanakotoka waandishi teule na lugha ngeni ili kuzalisha utanzu mseto ambao ni wa kimahuluti. Maoni haya ya Obiechina yanaafiki dhana kwamba umahuluti ni nguzo muhimu katika fasihi hasa fasihi ya Kiafrika. Chinweizu na Madubuike (1983) pia wamebainisha namna ambavyo athari za mitindo ya Ulaya zinazoibuka katika fasihi ya Kiafrika zimepelekea kuwepo kwa hali ya umahuluti. Kwa maoni yao, umahuluti huu umetokana na haja ya kukumbatia utamaduni wa Ulaya na kuutumia kama kigezo cha kueleza fasihi, ikiwemo fasihi ya Kiafriaka.

Kwa upande wake, Ngugi (1986) anazungumzia suala hili la umahuluti katika fasihi anapoeleza jinsi watunzi wengi wa fasihi ya Kiafrika walivyoamua kutumia lugha na mitindo ya lugha za Ulaya kueleza tajriba na hisia zao za Kiafrika. Waandishi hawa wamefanya hivyo kwa kuzirutubisha lugha hizo za Ulaya kwa vipengele vya fasihi simulizi ya Kiafrika kama vile matumizi ya methali na mifumo mahsusi ya usemi. Ametaja mifano ya watunzi kama vile Chinua Achebe, Amos Tutuola na Gabriel Okara kama waliochangia katika kubuni kazi za sanaa zilizo na sifa za kimahuluti zinazojumuisha tamaduni na mitindo ya Kiafrika na ile ya Ulaya.

Licha ya kazi hizo tangulizi kubainisha kuwepo kwa umahuluti katika fasihi ya Kiafrika, zimekijita katika suala la umahuluti unaotokana na athari ya fasihi simulizi ya Kiafrika katika tamaduni na lugha za Ulaya kupitia kazi za fasihi zilizoandikwa na watunzi wa Kiafrika. Watunzi hao wameandika katika lugha za Ulaya kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kireno lakini katika kufanya hivyo wakajumuisha vito vya tamaduni na fasihi simulizi za jamii zao za Kiafrika. Makala haya, hata hivyo, yamejikita katika suala la umahuluti unaotokana na athari ya tamaduni na lugha za Mwafrika dhidi ya Mwafrika. Kwa mujibu wa Sululu (2019), wapo waandishi wa Kiafrika wa riwaya ya Kiswahili ambao wamezingatia mandhari halisi kutoka jamii zao katika utunzi wa kazi za sanaa. Makala haya, hivyo basi, yamechunguza namna ambavyo umahuluti umejitokeza kupitia maelezo ya kisanaa yanayojumuisha mseto wa vipengele kutoka tamaduni za jamii tofauti wanakotoka watunzi wa Kiafrika. Mahsusi, makala haya yamechunguza suala la umahuluti kupitia uchunguzi wa riwaya teule ya Kiswahili iliyoandikwa na mtunzi wa Kiafrika asiyekuwa Mswahili.

**Mbinu za Utafiti**

Data iliyotumiwa kufanikisha makala haya ilikusanywa kutoka sehemu mbili: maktabani na nyanjani. Data kutoka maktabani ilipatikana kupitia usomaji wa kina wa riwaya ya *Mafuta* ili kubainisha matumizi ya tanzu za kimaigizo za fasihi simulizi, za jamii ya mtunzi teule, katika riwaya hii ya Kiswahili. Data hii, ambayo ilihusisha maneno, sentensi, vishazi na vifungu vilivyo na ukuruba na maelezo kuhusu tanzu za kimaigizo za fasihi simulizi ya mtunzi teule, ilinakiliwa na kutumiwa hatimaye katika uchanganuzi. Data kutoka nyanjani ilijumuisha tanzu za fasihi simulizi za jamii alikozaliwa na kukulia mtunzi teule ambaye riwaya yake ya Kiswahili ilichunguzwa katika utafiti huu. Data hii kutoka nyanjani ilipatikana kupitia matumizi ya mbinu za: hojaji na mahojiano ya ana kwa ana. Hojaji zilitumiwa kwa wahojiwa waliomfahamu kwa karibu Katama Mkangi ili kubainisha muktadha wa maisha ya mwandishi huyu, unaoambatana na umahuluti wa vipengele vya mazingira tofauti alimoishi na kukulia.

Kupitia mbinu ya mahojiano ya ana kwa ana, data iliyojumuisha masimulizi ya wahojiwa ya kipera cha *kuhala* (ndoa) cha utanzu wa kimaigizo wa fasihi simulizi ya jamii ya Waribe iliweza kupatikana. Data hiyo ilitumiwa kubainisha jinsi kipera hicho cha utanzu wa kimaigizo wa fasihi simulizi ya jamii ya mtunzi teule kilijibainisha katika riwaya ya *Mafuta* na hivyo kuchangia umahuluti wa riwaya hii ya Kiswahili.

Data yote iliyokusanywa kwa minajili ya uchunguzi huu ilichanganuliwa ili kubainisha namna ambavyo uingizaji wa kipera cha *kuhala* (ndoa) cha utanzu wa kimaigizo wa fasihi simulizi ya jamii ya mtunzi teule, asiyekuwa Mswahili, katika riwaya yake ya Kiswahili ulichangia umahuluti wa riwaya hii. Uchanganuzi huu ulifanywa kwa kuongozwa na lengo la makala haya ambalo ni kufafanua namna tanzu za kimaigizo za fasihi simulizi ya jamii ya Katama Mkangi zimechangia umahuluti wa riwaya ya Kiswahili, na mihimili ya Nadharia ya Umahuluti wa Utamaduni.

**Nadharia ya Umahuluti wa Utamaduni**

Tathmini hii iliongozwa na Nadharia ya Umahuluti wa Utamaduni. Nadharia hii inahusu fasihi na nadharia zinazotafiti na kuchanganua athari za mchanganyiko wa utambulisho wa utamaduni. Asili ya dhana umahuluti ni taaluma ya elimu-viumbe lakini baadaye ilijumuishwa katika utamaduni na isimu (Raab na Buttler, 2008). Nadharia ya Umahuluti wa Utamaduni, hivyo basi, ina misingi yake katika taaluma ya jenetiki ambayo ni kitengo cha elimu-viumbe. Kwa mujibu wa taaluma hii unapochanganya jeni tofauti, matokeo yake huwa bora kuliko unapochanganya jeni zinazofanana. Kwa misingi hiyo, mchanganyiko wa tamaduni tofauti huzaa utamaduni ambao ni bora na imara zaidi.

Bhabha (1994) ambaye ni mmojawapo wa waasisi wa nadharia hii, anaeleza umahuluti kama hali inayotokea wakati tamaduni mbili au zaidi zinapotagusana. Anafafanua kuwa, umahuluti ni dhana inayoashiria nafasi maalum ambapo mchakato wa mitagusano baina ya tamaduni mbalimbali hutokea. Naye Rosaldo (1995) anaeleza umahuluti kama hali inayoendelea daima katika tamaduni za binadamu wote. Ni hali ambayo inapinga kuwepo maeneo halisi yenye udhu kwa kuwa kila eneo hupitia mchakato huu wa mwingilianotamaduni unaohusisha ukopaji kutoka pande zote za tamaduni husika. Kwa hivyo umahuluti unatamalaki katika nyanja zote za maisha ya binadamu. Waitifaki wa nadharia hii kama vile Kraidy (2005) wanaeleza jinsi umahuluti ulivyokita mizizi katika jamii. Hivyo basi, taaluma mbalimbali katika maisha ya binadamu, zikiwemo fasihi na sanaa kwa ujumla, zimeshirikisha umahuluti kupitia njia ya mapokezano. Kwa hivyo, umahuluti ni dhana inayopinga hali ya uhalisi na kuwepo kwa namna moja ya vitu.

**Maigizo katika Jamii ya Waribe**

Data ya nyanjani kutoka eneo la Ribe, alikozaliwa na kukulia Katama Mkangi, ilidhihirisha kuwa fasihi simulizi ya jamii ya Waribe inasheheni utajiri mkubwa wa tanzu anuwai ukiwemo utanzu wa kimaigizo. Waribe wana utamaduni unaosheheni sherehe nyingi ambazo hufuata taratibu maalum. Sherehe hizi hufanyika nyakati mbalimbali na katika maeneo mahsusi. Taratibu za sherehe hizi huwajumuisha wanajamii wote, kila mmoja akielewa anachotarajiwa kutekeleza.

Mapitio ya riwaya ya *Mafuta*, yalibainisha matumizi ya tanzu za kimaigizo katika kazi hii ya sanaa ambayo yana mfanano mkubwa na baadhi ya tanzu za kimaigizo za fasihi simulizi ya Waribe. Mfanano huu umejitokeza kupitia tanzu kadhaa za kimaigizo mathalani *kuhala* (ndoa), jando, unyago, matambiko ya kaya, shughuli za marika, na shughuli za mahakama. Kati ya majukwaa haya mbalimbali ya kimaigizo, makala haya yalidadavua jukwaa la *kuhala* (ndoa) na jinsi vipengele vyake vya kimaigizo vya kifasihi simulizi vimechangia katika umahuluti wa riwaya teule ya Kiswahili iliyoandikwa na Katama Mkangi.

**_Kuhala_ (Ndoa)**

Kulingana na Nyamete, Buliba na Kamau (2016), ndoa ni ukamilifu wa makubaliano ya muungano wa mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mume na mke kulingana na sheria, mila au desturi za sehemu fulani. Asasi ya ndoa imepewa thamani kuu na Waribe kama ilivyobainika nyanjani. Hii ni kwa kuwa asasi hii ndiyo inayohakikishia jamii mwendelezo kupitia vizazi vyake mbalimbali. Hivyo basi, ni jukumu la kila mwanajamii wa Kiribe kutekeleza wajibu wake katika kufanikisha taratibu zote ambazo huchangia ufanisi wa asasi hii.

Zipo taratibu mbalimbali zinazohusisha utekelezaji wa *kuhala* (ndoa) katika jamii ya Waribe. Taratibu hizi hufuata ruwaza maalum kuanzia mwanzo ambapo vijana hupewa mafunzo kuhusu ndoa hadi kilele chake ambapo ndoa hufanikishwa kati ya wanandoa na familia zao. Taratibu hizi ziliongozwa na wanajamii teule ambao walielekeza kuhusu masuala muhimu ambayo yalistahili kuzingatiwa na wanajamii kuambatana na mila na desturi za jamii ya Waribe.

**Mchango wa Baadhi ya Vipengele vya _Kuhala_ (Ndoa) katika Umahuluti wa Riwaya ya _Mafuta_**

Katama Mkangi anatalii suala la ufanikishaji wa utanzu wa kimaigizo wa ndoa kwa kina. Katika jumuiya anayosawiri katika riwaya ya *Mafuta* kinachoibuka ni kuwa ndoa ni suala la kikati ambalo wahusika walilichukulia kwa uzito mkubwa. Miongoni mwa mambo mengine, mwandishi anaelekea kusisitiza suala la kuzingatiwa kwa taratibu ambapo msichana alitarajiwa kuwa bikra hadi kuolewa kwake. Kama anavyoeleza Osore (2016), hii ndiyo hali jinsi ilivyokuwa katika jamii nyingi za Kiafrika ambapo ni kupitia kwa ndoa pekee ambapo mwanamume aliweza kupata kibali cha kujuana kimwili na mkewe na hapo mkataba baina ya wawili hao ungechukuliwa kuwa mkataba kati ya jamaa zao vile vile. Kidesturi katika jamii ya Waribe, ni muhimu kwa wasichana na wavulana kutojuana kimwili kabla ya ndoa. Wote hufunzwa kujiheshimu na kuheshimiana ili ndoa zao ziwe zenye fanaka. *Tsangazimi*/*zimi* (shangazi) wa msichana ndiye anayetwikwa jukumu la kumfundisha msichana huyo kuhusu haja ya kutunza ubikra wake hadi wakati wa ndoa. Shangazi humnasihi msichana kwa kumwambia:

***Tsangazimi***: *Zimi, uchikala babayo bado kugwira mali, usijeze kulala na mulume maana ni makotsa! Koma tsindakulola vibaya*.

**Tafsiri**

**Shangazi**: Shangazi, kama babako hajashika mahari yako basi usithubutu kujuana kimwili na mwanamume yeyote. Ukikaidi na kufanya hivyo, wazee wako watakasirishwa na tendo hilo na kukushushia laana.

Maelekezo haya anayopewa msichana kusalia bikra hadi kuolewa kwake humkumbusha kuhusu jukumu muhimu alilonalo kwake mwenyewe, kwa familia na jamii yake kwa ujumla. Kwa sababu mafundisho haya ya shangazi huwa muhimu sana inafuatia kwamba baada ya ndoa, mume anapothibitisha kuwa msichana ni bikra hujukumika kutoa *kadzama* (zawadi) kwa shangazi kama ishara ya shukrani. Katama Mkangi anatoa taswira sawa na matarajio haya kwa vijana katika riwaya ya *Mafuta* kupitia kauli ya Mama Fofi ambaye anasimulia maisha ya ujana wake. Anaeleza:

> Posa, uchumba, na ndoa, vilitekelezwa kama desturi ilivyohitaji. Sifa mpenzi wangu ilimbidi akatoe heko kwa shangazi na wazazi wangu kwani hakunikuta na kasoro kamwe (uk. 28).

Kwa hivyo, maelezo katika riwaya teule yanaendana vizuri na data ya nyanjani kuhusu umuhimu wa vijana kutojuana kimwili kabla ya ndoa.

Vilevile, katika jamii ya Waribe, *wari* (wasichana) hupewa mafundisho ya kuwaandaa kwa majukumu mbalimbali ya ndoa. Mafundisho haya hufanywa unyagoni. Kule unyagoni, wasichana hukusanywa kwa minajili ya kupewa mafundisho kuhusu wajibu wao katika asasi ya ndoa. Hufundishwa na *nyakanga* (wanawake wenye umri mpevu na tajriba pana ya kimaisha). Miongoni mwa mambo wanayofundishwa ni utiifu kwa waume zao, uvumilivu, namna ya kutembea mbele ya watu na namna ya kuwalea watoto. Kuambatana na suala la utiifu kwa waume, kwa mfano, wasichana hao huasiwa ifuatavyo:

***Nyakanga***: *Uchenda kwa mulume wooo hakikisha unamtunza, unamheshimu, ichikalala ni ng'ombe babayo wezihala zisuye*.

**Tafsiri**

**Kungwi**: Ukienda kwa bwana yako hakikisha kwamba unamtunza, unamheshimu na usimwonyeshe dharau ili mahari ambayo baba yako atapewa isirejeshwe.

Aidha, msichana hushauriwa kuhusu umuhimu wa kuwa mvumilivu katika ndoa. Msichana huyo huambiwa:

***Nyakanga***: *Majembe kachikala hamwenga kagaricha. Lakini ichikala pengine uchikosana na mulume ni umsikize usikale dzulu na hasira. Usimikize arondakwambira. Echikala yudzikuudhi sema na babayo vyala*.

**Tafsiri**

**Kungwi**: Uelewe kuwa hata majembe yakiwekwa pamoja hugongana. Iwapo mmekosana usiongee kwa hasira au usije juu sana na kusababisha makabiliano. Ukiona kwamba mume wako amekukera sana basi zungumza na bavyaa wako kuhusu jambo hilo ili atumie busara yake kupata suluhu.

Wasichana pia hufundishwa namna ya kulinda watoto wao. Huambiwa:

***Nyakanga***: *Uchizyala mwana madzacha ni umwogese, umujitire muswa umukopoze. Achirira umbembeleze, usimuchemere*.

**Tafsiri**

**Kungwi**: Ukizaa mtoto hakikisha kwamba asubuhi umemuosha, umempa uji, umemlisha vizuri na akilia umbembeleze na wala usimfokee.

Kama wake, wasichana hawa hutarajiwa kuonyesha nidhamu katika maongezi, mavazi na hata kutembea kwao. Ndiposa wakaambiwa:

***Nyakanga***: *Uchikala unahisana na watu hakikisha mwenenzigo ni ga heshima*.

**Tafsiri**

**Kungwi**: Ukipishana na watu matembezi yako yawe ya heshima. Usinengue kiuno upishanapo na wazee wa rika la baba yako au bavyaa yako.

*Wari* (wasichana) wakishafundishwa kunga hizo zote na anayefundisha kuridhika kuwa yote muhimu yamepitishwa kwao basi watafuzu na kuondoka unyagoni. Wataambiwa:

***Nyakanga***: *Haya mmarigiza mafundisho genu. Endani mgagwire na mgatwirize*.

**Tafsiri**

**Kungwi**: Haya mmekamilisha mafundisho yenu. Sasa nendeni mkayatekeleze jinsi tulivyowafundisheni.

Hapo wasichana hao watakuwa tayari kuolewa na kuanzisha familia zao. Katika riwaya ya *Mafuta*, Katama Mkangi anatoa taswira ya hali kama hii kupitia kwa kauli ya Mama Fofi anayeeleza aliyopitia yeye mwenyewe. Anasema:

> Nilipelekwa kwa bibi mmoja huko, mimi pamoja na kumbo langu, tukatiwa jandoni. Tulifundishwa kuwa wanawake kikamilifu. Ustahimilivu na utiifu usio wa kikomo kwa wanaume, ndivyo vilivyosisitizwa kutwa kucha... Vipi kutembea kikazi na vipi kutembea kike… na mengi mengineyo ambayo lengo lake lilikuwa tuje tuwe wake wema nyumbani.

> Tulipofuzu, tulikuwa tayari. Tulikuwa tumedobea kanju kurudi nyuma! Lililosalia, ilikuwa ni kutundwa tu basi. Tulitawishwa, huku kila mmoja wetu akingojea aliyetunukiwa naye. Wangu akawa Sifa (uk. 28).

Mafundishio anayotaja Mama Fofi ni sawa na yale yanayojitokeza katika data ya nyanjani kuhusu walivyofanyiwa *wari* (wasichana) wa Kiribe wakiwa unyagoni. Kwa hivyo, usawiri wa mafundisho haya ya unyagoni na Katama Mkangi, kupitia mhusika Mama Fofi, ni mfano wa namna fasihi simulizi ya Waribe ilivyochangia uandishi wake wa riwaya teule ya Kiswahili na hivyo kuifanya riwaya hii kuwa ya kimahuluti.

Aidha, majukumu ya wakunga katika mchakato wa ndoa kama yalivyojitokeza katika data ya nyanjani yamejitokeza katika masimulizi ya Katama Mkangi katika riwaya ya *Mafuta*. Kwa mujibu wa maelezo ya nyanjani, msichana anapopata mimba hatimaye, mimba hiyo hutunzwa kwa uangalifu mpaka anapojifungua. Huwekwa chini ya uangalizi wa *mvyalusa* (mkunga) ambaye humwelekeza kuhusu vyakula anavyostahili kula na kumpa dawa kutoka kwa *mihaso* (miti mahsusi itumiwayo kama dawa*)* ili kuzuia ndwele za hapa na pale. Jukumu jingine muhimu analotekeleza mkunga, hasa kwa mwanamke ambaye ana ujauzito mara ya kwanza, ni kumhimiza asiwe na uoga. Humwambia:

***Mvyalusa***: *Usikale moga*

*Ni umuvyale mwangwa salama salimini. Usimushongole*.

**Tafsiri**

**Mkunga**: Usiwe mwoga, mzae mtoto wa watu salama salmini.

Isitoshe, siku ya kujifungua inapowadia mkunga hutekeleza jukumu muhimu la kufanikisha shughuli hiyo ya kujifungua. Kwanza, huhakikisha mazingira ya chumba cha kujifungulia yameandaliwa kidesturi. Mle chumbani huchomwa vipande vya mti uitwao *vumbani* ambao hutoa moshi wenye manukato. Moshi huo huondoa harufu yoyote mbaya mle chumbani. Mkunga vilevile hujukumika kumhimiza mama mjamzito kwa kumwambia :

***Mvyalusa***: *Piga pumzi tza tsini* !

**Tafsiri**

**Mkunga** : Pumua huku ukisukuma!

Ikiwa mama mjamzito ataonyesha uoga uliozidi basi mkunga atamzaba makofi makali hadi afanye analotakiwa kufanya ili kujifungua salama. Majukumu haya ya wakunga yanajitokeza katika riwaya ya *Mafuta* pale mwandishi anapoeleza kuwa Mama Fofi na mumewe, Sifa, walizaliwa kwa usaidizi wa wakunga. Mama Fofi anasema yafuatayo kuhusu kuzaliwa kwake:

> Mimi nilizaliwa godoroni, tena la usufi. Vyetezo vya ubani na vya udi vilikuwa vikining'inia mkunga aliponipokea. Moshi wa uvumba na manukato haya yote, ndio ulionialika hata kabla ya mkunga kunishtua kutoka kwa usingizi wa miezi tisa (uk. 27).

Naye Sifa, mumewe Mama Fofi, alizaliwa pia kwa usaidizi wa mkunga lakini mwandishi anatoa maelezo zaidi ya sherehe ya dhati ya makaribisho yake ulimwenguni. Katika jamii ya Waribe, baada ya kujifungua, mama mtoto hushinda ndani ya nyumba kwa siku kadhaa kisha baadaye humtoa mtoto nje rasmi katika sherehe inayoitwa *kumwombozandze mwana* (kumtoa mtoto nje). Ikiwa mtoto ni msichana, basi *kihiha* (kitita) kidogo cha kuni na *kaha* (kata) hufungiwa sehemu ya juu ya mlango anaopita mama na mtoto wakienda nje. Ikiwa ni mvulana basi hutiwa uta mdogo au kijembe kidogo. Vifaa hivi huashiria majukumu ambayo mtoto huyo hutazamiwa kutekeleza siku za usoni. Babu na nyanya yake mtoto pia humkaribisha ulimwenguni rasmi. Ikiwa kwa mfano babu yake mtoto anajulikana kama Katama basi humpa jina hilo mtoto huyo, ikiwa ni wa kiume, na kisha kumsemea maneno yafuatayo sikioni mwake:

***Tsawe***: *Katama, sinakondo na mtu mino washitoto na ndzio. Mubomu msena mpite msena*.

**Tafsiri**

**Babu** : Katama, mimi sina fujo na mtu. Hata nawe usiwe na fujo na mtu. Ishi vyema na wenzako.

Katama Mkangi, katika riwaya ya *Mafuta* anatoa maelezo kuhusu sherehe aliyofanyiwa Sifa ambayo ina ukuruba na sherehe ya *kumwombozandze mwana*. Mama Fofi anasimulia yafuatayo kuhusu kuzaliwa kwa Sifa:

> Kutoka tumboni mwa mamake, mkunga akazika vyalio lake pembeni humo nyumbani. Siku zake za kutolewa nje zilipofika, ni mlango huo huo ilimbidi apitishwe. Kufuatana na mila, mlangoni kuliwekwa uta, mshale, panga na jembe. Babuye Somoye alimshika sikio na akamunyunyizia dua la rehema, huku akimkabidhi vifaa vya jukumu lake 'sifa ndugu yangu', babuye akaanza, utokako hukujui na uendako pia. Hii ndiyo siri ya Mungu… Mimi somoyo, nimeshatolewa nje na ni afadhali nikupe ujuzi wangu mpaka wa leo…wewe kama mume basi yafaa ujitawale kwa kuvitawala vifaa hivi. Hebu basi nikurithishe vifaa hivi uje ubarikiwe navyo utakapovitumia… Hapa babuye akaviweka vile vifaa karibu naye… kama kumkaribisha, alichukua mwiba wa nungu akauchoma nchani na ukiwa na moto, akamchomachoma tumboni, viungoni na kwenye uti wa mgongo. Hivi ndivyo aliyekuwa mume wangu alivyoanza kuvuta hewa safi (kur. 25-26).

Sherehe hii ina ukuruba wa moja kwa moja na sherehe ya *kumwombozandze mwana* (kumtoa mtoto nje) kama ilivyoelezwa na wahojiwa nyanjani. Hii ni sherehe inayofanywa na Waribe siku chache baada ya mama kujifungua. Kwa hivyo, Katama Mkangi anatumia maelezo yanayojumuisha vito vya kimaigizo vya fasihi simulizi ya Waribe katika riwaya yake ya Kiswahili kwa upekee ambao umeirutubisha riwaya hii na kuifanya kuwa ya kimahuluti.

Licha ya kuwa suala la ndoa hujitokeza mara nyingi katika riwaya za Kiswahili, katika nyingi za riwaya hizo, hasa zilizoandikwa na waandishi ambao ni Waswahili, taratibu za utekelezaji wa ndoa hizo hufungamanishwa na masuala ya dini ya Kiislamu. Hii ni kwa kuwa Waswahili wengi ni waumini wa dini hiyo (Mbaabu, 1985). Hata hivyo, Katama Mkangi amelipa suala hili upekee kwa kuzingatia ufanikishaji wake kwa misingi ya hali jinsi ilivyo katika mila na desturi za Waribe. Amefanya hivyo kwa kushirikisha msururu wa matukio kama vile mafundisho ya *wari* (wasichana) na *tzangazimi* (shangazi), posa na kutoa *kadzama* (zawadi), *kuhasa* (kubariki), wajibu wa *mvyalusa* (mkunga) na *kumwombozandze mwana* (kumtoa mtoto nje). Taratibu hizi zimeshabihi namna wafanyavyo Waribe katika ufanikishaji wa miviga hii ya kimaigizo kulingana na maelezo ya wahojiwa nyanjani. Kwa hivyo, taratibu mbalimbali zinazoambatana na ufanikishaji wa asasi ya ndoa kama zilivyotumiwa na Katama Mkangi na mfanano wake na maelezo yanayojumuisha data ya nyanjani kuhusu utanzu huu katika jamii ya Waribe zinadhihirisha jinsi tanzu za kimaigizo za fasihi simulizi ya Waribe zilivyochangia muundo anaotumia Katama Mkangi kufanikisha riwaya yake teule ya Kiswahili. Kwa hivyo, mchango wa utanzu huu wa kimaigizo umeiendeleza riwaya hii ya Kiswahili na kuifanya kuwa ya kimahuluti.

**Hitimisho**

Kwa ujumla, kipera cha utanzu za kimaigizo cha *kuhala* (ndoa), kama kilivyosawiriwa katika riwaya teule ya Katama Mkangi, kinaelekea kushabihiana na maadhimisho sawia ya kipera hicho cha kimaigizo kama kilivyobainishwa na wahojiwa kutoka katika jamii ya Waribe. Ni sawa basi kusema kuwa fasihi simulizi ya jamii ya mtunzi huyu imechangia katika uandishi wa riwaya yake ya Kiswahili. Mchango huu umebainishwa kupitia kwa muundo wa riwaya hii ambao unasheheni utajiri mkubwa wa matumizi ya maigizo. Hali hii inaafiki maelezo ya nadharia ya Umahuluti wa Utamaduni kwamba katika kipindi cha kisasa pameshuhudiwa ongezeko la hali ya mtagusano wa kitamaduni baina ya jamii mbalimbali ambao unahusisha mapokezano ya mambo yanayohusu jadi, maadhimisho na miviga ambayo ni sehemu ya maisha ya kila siku ya wanajamii katika jamii hizo. Katama Mkangi anadhihirisha hali hii kupitia kwa uingizaji wake wa usanii wa ufanikishaji wa kipera cha utanzu wa kimaigizo cha *kuhala* (ndoa), katika riwaya yake teule ya Kiswahili. Amefanya hivyo kwa usanii wa kipekee ambao unapelekea utanzu huo wa kifasihi kuwa sehemu ya masimulizi na muundo wa riwaya

ya Kiswahili ya *Mafuta* na kwa njia hiyo kuchangia umahuluti wa riwaya hii na riwaya ya Kiswahili kwa ujumla.

**Marejeleo**

Bhabha, H. K. (1994). *The Location of Culture*. New York: Routledge.

Chinweizu, O. J. & Madubuike, I. (1983). *Towards the Decolonization of African Literature*. Washington D.C.: Howard University Press.

Kraidy, M. (2005). *Hybridity or the Cultural Logic of Globalization*. Philadelphia: Temple.

Maritim, E. (2012). 'The Concept and Nature of Drama and Theatre in Traditional African Societies.' in: *African Drama & Theatre A Criticism*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing Co. Ltd.

Mkangi, K. (1984). *Mafuta*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Nyamete, F., Buliba, F. A. & Kamau, N. G. (2016). 'Ufafanuzi wa Vichocheo vya Migogoro ya Kindoa kama Vinavyosawiriwa katika Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na Ken Walibora' katika *International Journal of Advanced Education and Research Volume 1; Issue 9*; Pgs. 19-27. Retrieved from http://www.alleducationjournal.com on 21st September, 2020.

Obiechina, E. (1975). *Culture, Tradition and Society in the West African Novel*. Cambridge: Cambridge University Press.

Okwena, S. (2019). "Umahuluti wa Miundo katika Tamthilia za Ibrahim Hussein". Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Osore, M. K. (2016). 'Defamiliarizing Marriage in a Patriarchal Socio-Cultural Context: An Analysis of the Novels of Euphrase Kezilahabi and Said Ahmed Mohamed' in: *Kiswahili. Juz 79*: Pgs. 28-42. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Raab, J. & Buttler, M. (2008). *Hybrid Americas: Contracts, Contrasts and Conferences in New World Literatures and Cultures*. Verlag. Tempe: Bilingual Press.

Rosaldo, R. (1995). "Foreword" in: *Hybrid Cultures: Strategies for Entering and Leaving Modernity* (Nestor Garcia Canclini). Tafsiri: Chiappari, C.L & Lopez, S.L. Minneapolis: University of Minnesota Press.

Sululu, B. S. (2019). 'Riwaya ya Kiswahili Kama Utanzu Mahuluti: Mfano wa Riwaya ya *Ndoto ya Almasi*.' Katika, *Uwezeshwaji wa Kiswahili Kama Wenzo wa Maarifa*. Eldoret: Moi University Press. Kur. 235-242.

Sululu, B. S., Wafula, R .M. & Maitaria, J. N. (2021). 'Mchango wa Tanzu za Kimaigizo za Fasihi Simulizi katika Umahuluti wa Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi wa Riwaya ya *Kufa Kuzikana*.' Katika, *East African Journal of Swahili Studies*. *Vol.3 (1)*. Kur. 91-99.

Sululu, B.S. (2021). "Umahuluti wa Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi wa Riwaya Teule za Ken Walibora na Katama Mkangi." Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Wa Thiong'o, N. (1986). *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.